JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**
ISO 9001:2015 CERTIFIED

**KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM**

**SHAURI NA. 07 - 2020/2021**

**DHIDI YA**

# CG FM RADIO

# UAMUZI

**UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU TUHUMA ZA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA UTANGAZAJI WA REDIO NA TELEVISHENI), 2018**

## 1.0 MAELEZO KUHUSU UKIUKAJI WA KANUNI

1.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilitoa leseni ya kutoa huduma ya utangazaji kwa **CG FM Radio** ili kutangaza habari mbali mbali kwa njia ya redio.

1.2 Kituo cha utangazaji cha **CG FM Radio** cha Tabora kinatuhumiwa kukiuka Agizo la Serikali lililotolewa tarehe 03 Mei, 2017 ambalo linawataka watangazaji wa vituo vya Redio na Televisheni kutosoma maudhui yaliyopo katika magazeti kwa undani na badala yake wasome vichwa vya habari pekee.

1.3 Tarehe 15 Juni, 2017 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania iliviandikia barua Vituo vyote vya Utangazaji na kuvitaka kutekeleza Agizo hilo. Lengo la Agizo la Serikali ni kulinda ushindani wa kibiashara katika tasnia ya habari.

1.4 Kituo cha **CG FM Radio** kimekiuka Agizo la Serikali kupitia kipindi chake cha **Morning Power** ambacho kilirushwa tarehe 01 Julai, 2020 kati ya Saa 1.00 na Saa 3.30 Asubuhi. Katika kipindi hicho, mtangazaji alisikika akisoma kwa undani na kujadili habari mbali mbali zilizoandikwa katika magazeti, kinyume na Agizo lililotolewa na Serikali.

1.5 Kituo cha **CG FM Radio** kimekiuka na kupuuza kwa makusudi Agizo la Serikali pale mtangazaji wa kipindi cha **Morning Power** alipokuwa akisoma kwa undani na kujadili habari mbali mbali zilizoandikwa katika magazeti. Mtangazaji alisoma kwa undani habari za magazetini kama ifuatavyo:

***Nipashe:***

*Wagombea ruksa kujipitisha wanasema CCM, JPM aanika sababu za kuwania tena akerwa wasaka urais Zanzibar kuchafuana habari ukurasa wake wa pili lakini Zitto amkaribisha Membe upinzani habari ukurasa wake wa pili gazeti Nipashe*

*Kwamba kiongozi wa chama cha ACT- Wazalendo, Zitto Kabwe amesema sasa ni wakati muafaka kwa Bernard Membe kujiunga na vyama vya upinzani.*

*Akizungumza katika mkutano wa hadhara uliofanyika Kilwa mkoani Lindi jana Zitto alisema mwanasiasa huyo aliyewahi kuwa Mbunge na Waziri wa Wizara nyeti nchini ana fursa ya kuwaunganisha watanzania wenye kiu ya mabadiliko kupitia vyama mbadala vya siasa.*

***Maoni ya wahariri gazeti la Mwananchi***
*Dharura inahitajika tatizo la usafiri wa wanafunzi*

*Shule za awali hadi kidato cha tano zimefunguliwa kuanzia juzi tangu zilipofungwa Machi 17, 2020 baada ya mgonjwa wa Covid 19 aliporipotiwa nchini Machi 16, 2020, tahadhari kadhaa zimechukuliwa kukabiliana na maambulkizi ya Corona ikiwemo uvaaji barakoa, unawaji mikono kwa maji tiririka na kupimwa joto la mwili.*

*Mamia kwa maelfu ya wanafunzi wamerejea shule huku kukiwa kuna utekelezaji wa agizo la kuchukua abiria kulingana na idadi ya viti ndani ya vyombo vya usafiri.*

*Agizo hilo lilitolewa na Mamlaka ya Udhibiti na Usafiri wa Ardhi (LATRA) ambalo ni miongoni mwa jitihada za kudhibiti maambukizi ya ugonjwa wa Covid 19.*

*Licha ya kuwa muhimu kwa usafiri wa kistaarabu na kiafya limesababisha changamoto ya usafiri kwa wanafunzi.*

*Uchunguzi wa gazeti hili katika miji mikuu na mikoa mbalimbali nchini juzi na jana imeshuhudia adha ya usafiri kwa wanafunzi hasa wa shule za umma na shule binafsi ambao wazazi wao hawamudu kuwalipia gharama za magari ya shule ambao kutwa nzima walijazana vituoni bila matumaini ya kupata usafiri.*

*Mfano katika vituo vya Mbande, Mbagala, Mtongani, Tandika, Buguruni na Ilala Boma jijini Dar es Salaam. Vituo vya Nyegezi, Mkuyuni, na hata Posta Igombe na Nyakato jijini Mwanza wanafunzi wengi walitumia hata zaidi ya saa mbili kuhangaikia usafiri wa kwenda shule.*

*Mhariri ameongea mengi hapa lakini mwisho anasema katika hili sio serikali pekee ina dhamana bali pia wazazi, walezi na uongozi wa shule kila mmoja kwa uwezo nafasi na eneo lake atimize wajibu tuwawekee mazingira bora*

*watoto wetu wanapotekeleza wajibu wao wa kwenda shule kusoma anamaliza hivyo mhariri wa gazeti Mwananchi.*

*Lakini kwenye kibonzo hapa wanafunzi wakiwa wamevaa barakoa hii barakoa ambayo wameivaa hapa inaonekana ameivaa mpaka usoni mpaka macho hayaoonekani halafu wanaelekea kwenye kibao kimeandikwa shule. Ni maoni gazeti Mwananchi na kibonzo chake.*

*Kwa upande wa gazeti **Uhuru** mhariri anasema kwamba upatikanaji umeme vijijini uboreshe maisha ya wananchi.*

*Kwa upande wa gazeti **Nipashe** siku ya leo mhariri anasema umakini unahitajika katika utekelezaji wa bajeti ya 2020/2021. Kwenye kibonzo hapa kuna watu wamevaa suti amebeba furushi limeandikwa zawadi halafu amevaa suruali imeandikwa mtia nia anaelekea kumpigia magoti mtu ameandikwa sisi halafu huku kuna kwa nyuma ya huyu mtu aliyebeba zawadi kuna lisamaki likubwa limeandikwa TAKUKURU. Ni maoni mhariri gazeti la Nipashe na Kibonzo chake.*

## 2.0 UKIUKWAJI WA AGIZO

Kitendo cha kusoma na kuchambua kwa undani habari zilizoandikwa kwenye magazeti, Kituo cha **CG FM Radio** kinatuhumiwa kupuuza kwa makusudi Agizo la Serikali la tarehe 03 Mei, 2017.

## 3.0 WITO WA KUTOA MAELEZO YA UTETEZI

Tarehe 27 Julai, 2020, Kamati ya Maudhui iliuandikia uongozi wa **CG FM Radio,** wito wa kuwasilisha utetezi wao wa maandishi pamoja na kufika mbele ya Kamati ya Maudhui kujieleza kwa nini wasichukuliwe hatua kwa kukiuka Agizo hilo.

Tarehe 06 Agosti, 2020, Uongozi wa **CG FM Radio** uliwasilisha utetezi wa maandishi uliosainiwa na **Charles George Tihailwa**, Mkurugenzi wa Kituo. Pia, tarehe hiyo hiyo Uongozi huo ukiwakilishwa na **Charles George** ulifika mbele ya Kamati kutoa utetezi.

## 4.0 KUSOMEWA SHITAKA NA KUSIKILIZA MAUDHUI YA CG FM RADIO

Kamati ya Maudhui iliusomea Uongozi wa **CG FM Radio** shitaka lao. Pia, Kamati ya Maudhui na Uongozi wa **CG FM Radio** walisikiliza maudhui yaliyotangazwa na kulalamikiwa. Baada ya hapo Uongozi wa **CG FM Radio** ulipewa nafasi ya kujitetea.

## 5.0 UTETEZI WA CG FM RADIO

Katika maelezo yao utetezi kwa maandishi**, CG FM RADIO** walikiri kosa la kukiuka Agizo la Serikali na waliomba radhi. Walisema kuwa kosa halikutendeka kwa makusudi bali mtangazaji wao alipitiwa.

Waliendelea kusema kuwa ni desturi yao kuwahimiza na kuwafuatilia watangazaji ili wafuate maelekezo, Sheria, Kanuni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari.

Walieleza kuwa wamempa onyo mtangazaji aliyesababisha kosa hilo na kusema kwamba ameahidi kutolirudia kosa.

Walihitimisha utetezi wao kwa ahadi ya kuendelea kusimamia na kutekeleza Sheria, Kanuni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari.

Pia, **CG FM RADIO** ilitoa utetezi wa mdomo kama ifuatavyo:

Bwana **Charles George** aliendelea kukiri kosa na akaomba radhi akisema kuwa kosa lililotendeka ni la kibinadamu kwani mtangazaji alijisahau.

Aliendelea kusema kuwa kutokana na janga la Corona, vikao vya wafanyakzi wote vya Ijumaa havikuwa vikifanyika na hivyo kusababisha mtangazaji wao kujisahau. Alisema kuwa mtangazaji aliyehusika ana uzoefu, anajitambua na ni mtaalamu wa Utangazaji.

Alihitimisha utetezi wake kwa ahadi ya kusimamia maudhui ya kituo chake vizuri zaidi.

## 6.0 TATHMINI YA KAMATI

6.1 Kamati ya Maudhui imebaini kuwa **CG FM RADIO** wametenda kwa uzembe kosa la kusoma na kuchambua kwa undani habari zilizoandikwa kwenye magazeti kinyume na Agizo la Serikali.

6.2 Kamati ya Maudhui pia imejiridhisha kuwa **CG FM RADIO** wana usimamizi dhaifu wa vipindi vyao. Hili limedhihirika wakati wakiulizwa maswali na Kamati ambapo wamethibitisha kuwa walikuwa hawakifuatilii kwa karibu kipindi kilichohusika kwa kuamini kuwa mtangazaji mhusika ni mzoefu na anazijua taratibu.

## 7.0 USHAURI WA KAMATI KWA CG FM RADIO

7.1 Kutokana na makosa yaliyobainika, Kamati inaushauri Uongozi wa **CG FM RADIO** kuimarisha usimamizi wa vipindi vyao ili kuepuka uvunjaji wa Sheria, Kanuni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari;

7.2 **CG FM RADIO** wanashauriwa kuwapatia watangazaji wao na wasimamizi wa vipindi, mafunzo ya mara kwa mara juu ya Sheria, Kanuni na Maadili ya Utangazaji wa Habari kwa ujumla ili wapate matokeo chanya katika kazi zao.

## 8.0 UAMUZI WA KAMATI

Baada ya kuutafakari kwa kina utetezi uliotolewa na Uongozi wa **CG FM RADIO**, Kamati ya Maudhui imeridhika pasi na shaka kuwa **CG FM RADIO** wamekiuka kwa uzembe na kwa makusudi Agizo la Serikali, linalozuia kusoma kwa undani habari za magazetini.

Hivyo basi, Kamati ya Maudhui inatoa adhabu zifuatazo kwa **CG FM RADIO:**

1. Wanapewa Onyo;
2. Wanawekwa chini ya uangalizi kwa muda wa miezi mitatu (3) pamoja na kutahadharishwa kuwa hatua kali zaidi za kisheria zitachukuliwa dhidi yao iwapo hawatajirekebisha ndani ya muda tajwa.

Uamuzi huu umetolewa Dar es Salaam, leo tarehe **14 Agosti, 2020**.

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia siku ya kusomwa kwa uamuzi huu.

**Uamuzi huu umesainiwa na:**

**Joseph Method Mapunda**

..................................................................

**Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

**PAMOJA NA WAJUMBE WAFUATAO WA KAMATI YA MAUDHUI:**

1. **Abdul Ramadhani Ngarawa** ..............................
2. **Derek Kaitira Murusuri** ..............................
3. **Jacob Gregory Tesha** ..............................